KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 11, Issue 2

10th RAJAB 1432

3rd June, 2011

YALIYOMO

MWEZI WA RAJAB 1 - 4

FATAAWA 4

MWEZI WA RAJAB

Mtayarishi: Sheikh Muhammad al-Munajjid

Kila sifa njema ni zenye kumthubutukia Allaah (سبحانه وتعالى), na Baraka na Amani zimshukie Mtume Mteule, pamoja na ahli zake walio bota na waliotakaswa, na Maswahaba zake.

Ametukuka Allaah (سبحانه وتعالى) aliyesema (kulingana na tafsiri): **"Na Mola wako huumba atakavyo na huchagua (atakavyo)."** [Al-Qasas (28): 68]. Sifa hii ya kuchagua au kukagua ni yenye kuashiriya Uola na Upwele Wake, na ukamilifu wa Hikma yake, 'Ilmu yake na Nguvu zake. Kipengele kimoja cha uchaguzi na upendeleo wake ni uhakika yakwamba amechagua baadhi ya masiku na miezi na na kuyapa ubora kuliko mengine. Miongoni mwa miezi. Allaah amechagua minne ambayo aliyoyafanya kuwa ni mitukufu, kama alivyosema (سبحانه وتعالى) (kulingana na tafsiri): **"Idadi ya miezi (ya mwaka mmoja) mbele ya Allaah ni miezi kumi na mbili katikan ilimu ya Allaah (mwenyewe tangu) siku alipoumba Mbingu na Ardhi. Katika hiyo imo minne iliyo mitukufu kabisa (nayo ni Rajab, mfungi pili, mfungo tatu, na mfungo nne). (Kufanya) hivi ndio Dini iliyo sawa. Basi msijidhulumu nafsi zenu ..."** [at-Tawbah (9):36].

قافلة الرحمة للحج والعمرة Al-Rahma `Umrah & Hajj

Agencies1432 Hijri / 2011 C.E

Assalaamu `Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah Safari yetu ya mwaka huu 1432 Hijri/2011 ya kupeleka watu `Umrah katika mwezi wa Ramadhaan, kumi la mwisho. Na vilevile katika `Ibaadah ya Hijjah.

Mipangilio ya Safari ya `Umrah (Mwezi wa Ramadhaan) ni kama ifuatayo:

• Kuondoka ni tarehe 17 ya mwezi wa Ramadhaan*Kurudi ni baada ya `Eid Insha Allaah

• Safari itaanzia Nairobi – Jeddah

• Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli na Usafiri) ni $1500 U.S

• Siku tatu tutakuwa Madinah na Siku kumi za mwisho tutakuwa Makkah mpaka `Eid.

• Safari ya Kurudi Jeddah – Nairobi. Itakuwa baada ya `Eid

Twapenda kuwahimiza wale wale wenye niya ya kwenda na sisi waharakishe kuleta Passport zao na picha Nne kwa ajili ya kufanya maandalizi. Sababu ni kwamba Viza zitafungwa kabla ya mweizi wa Ramadhaan kuanza.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa njia zifuatazo:

• Tutumie e-mail katika info@qssea.net au

• Simu nambari +254 723471820 (Abu Bilaal Athman Na'man)

• Simu nambari +254 721473181 (Abu Farida Muhammad Basawad)

FATAAWA

Miezi hii imehisabiwa kulingana na mizunguko ya mwezi, na wala si mizunguko ya jua, kama wafanyavyo Makafiri. Miezi mitukufu imetajwa kwa kuhusishwa katika Qur'an, lakini majina hayakutajwa. Majina yake yametajwa kwenye Sunnah: Imepokewa kutoka kwa Abu Bakrah (رضي الله عنه) yakwamba, Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) alitoa khutbah yake ya mwisho na akasema: "*Wakati ushakamilisha mizunguko yake na sasa ni kama ilivyokuwa katika siku ambayo Allaah alipoziumba Mbingu na Ardhi. Mwaka ni miezi kumi na mbili, ambayo minne yake ni mitukufu, miezi mitatu ya kufuatana –Dhul-Qa'dah, Dhul-Hijjah na Muharram—na Rajab ya Mudar ambayo hutokea baina ya Jumaada na Sha'baan.*" [Imepokewa na al-Bukhaari, No. 1741, katika [Kitaab] al-Hajj, al-Khutbah Ayaam Mina; na Muslim No. 1679 katika [Kitaab] al-Qisaamah, Baab Tahreem ad-Dimaa']. Imeitwa Rajab ya Mudar kwa sababu [kabila la] Mudar lilikuwa halina machezo na nyakati, kinyume na Waarabu wengine, waliokuwa wakifanya machezo na kutojali kuhusu miezi na kubadilisha mipangilio yake kulingana na hali walizokuwa nazo za kivita au laa. Huku ndiko kubadilisha kulikokusudiwa kwenye Aya (kulingana na tafsiri): **"Bila shaka kuakhirisha (miezi mitukufu isije upesi) ni kuzidi katika ukafiri; kwa hayo hupotezwa wale waliokufuru; wanaohalalisha (mwezi mtukufu), mwaka mmoja na kuuharamisha mwaka (mwengine), iliwafanye kuwa sawa idadi ya ile (miezi) aliyoitukuza Allaah (aliyoiharamisha Allaah); kwa hivyo huhalalisha alivyoviharamisha Allaah."** [at-Tawbah (9): 37].

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

Imesemwa yakwamba sababu iliyofanya kunasibishwa na Mudar ilikuwa ni kwamba wao (Mudar) waliiheshimu na kuitukuza sana, kwahivyo ikanasibishwa nao.

SABABU YA KUITWA KWA JINA HILO (RAJAB)

Ibn Faaris, amesema katika *Mu'jam Maqaayees al-Lughah* (Uk. 445): Herufi *Ra', jeem na ba'* hujenga mzizi wenye kuashiriya usaidizi na kutilia nguvu kitu kwa kitu chengine. ... Kwahiyo tamshi "*Rajabtu'l-shay*" lina maana yakwamba nimeitukuza ... Iliitwa Rajab kwa sababu walikuwa wakiitukuza, na vilevile imetukuzwa katika Sharee'ah. Katika zama za Jaahiliyyah, watu walikuwa wakiita Rajab *Munassil al-Asinnah* [jambo lenye kusababisha kung'olewa vichwa vya silaha vyenye makali], kama ilivyopokewa yakwamba Abu Rajaa' al-Ataaridi amesema: "Tulikuwa tukiabudu jiwe, kisha baada ya muda tukipata jiwe jengine zuri kuliko lile la kwanza, tuliwachana nalo tukashika hilo jengine. Iwapo hatukupata jiwe, twakusanya ghasiya (takataka), kisha huleta kondoo jike tukamnyonyesha maziwa kwenye zile ghasiya, kisha twafanya Twawaaf kumzunguka hapo. Unapoingia mwezi wa Rajab, tulikuwa tukisema *Munassil al-Asinnah* [jambo lenye kusababisha kung'olewa vichwa vya silaha vyenye makali], na tukawa hatuwachi mkuki wowote au mshale wenye kipande cha chuma isipokuwa tulikuwa tuking'oa kichwa chake cha chuma na kukiweka kando kwenye mwezi wa Rajab [Imepokewa na al-Bukhaari].

JIPATIE NAKALA YA KITABU CHA SWALA:

NAMBARI ZA SIMU NI:

0721473181 AU 0727341779

MOMBASA

Amesema al-Baihaqee: "Watu katika zama za Jaahiliyyah walikuwa wakipenda kuitukuza hii miezi mitukufu, haswa mwezi wa Rajab, na walikuwa hawapigani katika mwezi huu.

RAJAB NI MWEZI MTUKUFU

Miezi mitukufu ina daraja maalum, yenye kuihusu vilevile Mwezi wa Rajab kwa sababu nao ni miongoni mwa hiyo miezi mitukufu. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) (kulingana na tafsiri): **"Enyi mlioamini! Msivunje heshima ya alama za (dini ya) Allaah wala (heshima) ya mwezi uliotukuzwa ..."** [al-Maa'idah (5):2]. Hii ina maana yakwamba: Musiukhalifu utukufu wale ambao Allaah aliowaamrisha nyinyi muuheshimu na kuwakataza musiukhalifu, kwani kukatazwa huku kunahusu matendo mabaya na imani potofu.

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) (kulingana na tafsiri): **"Basi msijidhulumu nafsi zenu (kwa kufanya ma'asi) katika (miezi) hiyo ..."** [at-Tawbah (9): 36], ikimaanisha, kwenye miezi mitukufu. Neno hili "*Fee-Hinna*" iliyofasiriwa hapa kama ["*katika (miezi) hiyo*"] imekusudiwa miezi hii minne mitukufu, kama ilivyoashiriwa na Imaam wa Mufassireen, Ibn Jareer at-Twabaree (رحمه الله).

Kwahivyo tunatakikaniwa kuwa na tahadhari hapa na hii miezi minne, kwa sababu Allaah ameyakhusisha kando kwa daraja maalum na akatukataza kufanya ma'asi kwa ajili ya kuuheshimu utukufu wake, kwanin ma'asi yanayotekelezwa kwenye wakati huu ni maovu zaidi, kwa sababu ya utukufu wa wakati ambao Allaah alioutukuza.

Kwahiyo, katika Aya iliyotangulia hapo juu, Allaah ametukataza tusijidhulumu nafsi zetu, hata kama jambo hili—yaani; kujidhulumu nafsi zetu, ni lenye kuhusu kutenda madhambi - limekatazwa katika miezi yote ya mwaka mzima.

KUPIGANA KATIKA MIEZI MITUKUFU

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) (kulingana na tafsiri): **"Wanakuuliza (hukumu ya) kupigana vita katika miezi mitakatifu. Sema: "Kupigana vita katika (miezi) hiyo ni dhambi kubwa. ..."** [al-Baqarah (2):217]. Jamhuri kubwa ya wanavyuoni wamesema yakwamba hukmu ya (kukatazwa) kupigana katika miezi mitukufu imefutwa na Aya isemayo (kulingana na tafsiri): **"Na ile miezi mitukufu itakapokwisha (Ile miezi minne waliyopewa), basi wauweni (piganeni na) washirikina popote muwakutapo ..."** [at-Tawbah (9): 5] na Aayaat nyengine na hadeeth ambazo ni za ujumla katika matumizi yake na ambazo ni zenye kuhusisha maamrisho ya kuwapiga vita.

Wengine wamesema, hairuhusiwi kuvianzisha vita katika miezi mitukufu, lakini inaruhusiwa kuendelea na kumaliza kupigana, ikiwa vita vilianza katika wakati tafauti. Vita alivyopigana Mtume (صلى الله عليه وسلم) dhidi ya watu wa Taa'if vimefafanuliwa kwa njia hii, kwa sababu vita vilianzia Hunayn katika mwezi wa Shawwaal.

Yaliyotajwa hayahusiani na kupigana vita vya kujihami. Iwapo adui ataazisha mashambulizi kwenye ardhi za Waislamu, ni waajib juu ya wakaazi kujihami nafsi zao, emma hayo yatokeapo katika miezi mitukufu au laa.

AL-'ATEERAH (Sampuli ya Sadaka)

Katika zama za Jaahiliyyah, waarabu walikuwa wakichinja mnyama kwa ajili ya swadaka katika mwezi wa Rajab, kama kitendo cha ibada kwa masanamu yao. Ulipokuja Uislamu na mafundisho yake kwamba swadaka zinastahili kutolewa kwa ajili ya Allaah Peke yake, kitendo hichi cha ki-Jaahiliyyah kikaondolewa mbali. *Ma-Fuqahaa'* wakakhitilafiana kuhusiana na hukmu kuhusu kutoa swadaka katika mwezi wa Rajab. Kundi kubwa la *ma-Hanafee*, *Maalikee* na *ma-Hanbalee* wamesema yakwamba hukmu ya swadaka ya al-'*Ateerah* imeondolewa. Ushahidi wao ni hadeeth isemayo: "*Hakuna Fir', na wala hakuna 'Ateerah.*" [Imepokewa na al-Bukhaari na Muslim kutoka kwa Abu Hurairah]. *Ma-Shaafi'ee* wamesema yakwamba hukmu kuhusiana na *al-'Ateerah* haikuondolewa, na wakalichukulia yakwamba ni jambo *Mustahabb* (lenye kupendekezwa). Hii pia ndiyo iliyokuwa rai ya Ibn Sireen. Amesema Ibn Hajar: "Hii imeungwa mkono na hadeeth iliyopokewa na Abu Daawud, an-Nasaa'ee na Ibn Maajah, na ikaorodheshwa kuwa ni swaheeh na al -Haakim na Ibn al-Mundhir, kutoka kwa Nubayshah, aliyesema: 'Mtu mmoja alikwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: "Sisi tulikuwa

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

tukitoa swadaka (tukichinja) al-'Ateerah wakati wa u-jaahiliyyah kwenye mwezi wa Rajab.
Watuamrisha nini? Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): Toeni swadaka (chinjeni), pasi na kujali ni mwezi gani huo ..."
Ibn Hajar akasema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuipiga marufuku ki-Msingi, lakini alipiga marufuku ile fikra ya kuchinja huku ukafanywa makhsusi katika mwezi wa Rajab."

KUFUNGA KATIKA MWEZI WA RAJAB

Hakuna riwaya yoyote iliyo swaheeh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au kutoka kwa Swahaba yenye kuashiriya yakwamba kuna fadhla zozote za kufunga katika mwezi wa Rajab. Saumu iliyoamrishwa kwenye mwezi wa Rajab ni sawa na saumu iliyoamrishwa katika miezi mengine, kwa majina kufunga siku za Jumatatu na Alkhamisi, na sikun tatu za *al-Beedh* (siku nyeupe), saumu za siku moja na kuacha siku ifuatayo, na sumu ya *Siraar ash-Shahr*. Baadhi ya wanavyuoni wamesema yakwamba *Siraar ash-Shahr* imekusudiwa mwanzoni mwa mwezi, na baadhi nyengine wamesema yakwamba imekusudiwa kati-kati au mwishoni mwa mwezi. 'Umar (رضي الله عنه) alikuwa akikataza watu kufunga katika mwezi wa Rajab kwa sababu ya inahusisha kujifananisha na U-jaahiliyyah. Imepokewa yakwamba Kharashah ibn al-Harr amesema: "Nilimuona 'Umar akiinusa mikono ya waliokuwa wamefunga katika mwezi wa Rajab, mpaka wakawa ni wenye kutafuta chakula, na huku akisema, Huu ni mwezi uliotukuzwa kwenye zama za Jaahiliyyah. [*al-Irwaa'*, 957; al-Albaani amesema yakwamba ni swaheeh].
Amesema Imaam Ibn al-Qayyim: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kufunga kwa miezi mitatu mfululizo (yaani; Rajab, Sha'baan na Ramadhaan) kama wanavyofanya baadhi ya watu, hakuwahi kufunga Rajab kabisa na wala hakuwahimiza watu kufunga katika mwezi huu."
Al-Haafidh ibn Hajar amesema katika *Tabayyun al-'Ajab bimaa wurida fee fadhl-Rajab:* "Hakuna hadeeth yoyote iwezayo kutumika kama dalili iliyopokewa kuhusiana na fadhla za mwezi wa Rajab au kufunga mwezi huu au kufunga katika sehemu yoyote makhsusi ya mwezi huu, au kutekeleza Qiyaam Ul-Layl khususan katika mwezi huu. Imaam Abu Isma'eel al-Harawee al-Haafidh ametangulia kuyasema haya kabla yangu, na pia sisi tumeyanukuu haya kutoka kwa wengine.
Katika *al-Fataawa al-Lajnah ad-Daa'imah* imenukuliwa: "Ama kuhusu kufunga katika mwezi wa Rajab, sisi hatujui ni kwa misingi yapi kwenye Sharee'ah ya kufanya hivyo."

UMRAH KATIKA MWEZI WA RAJAB

Ahaadeeth zinaashiriya yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakufanya 'Umrah katika mwezi wa Rajab, kama ilivyopokewa yakwamba Mujaahid amesema: "Mimi na 'Urwah ibn az-Zubayr tuliingia msikitini na hapo tukamkuta 'Abdullaah ibn 'Umar amekaa karibu na chumba cha 'Aaisha (رضي الله عنها). Akaulizwa: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifanya 'Umrah mara ngapi?" Akajibu: "Mara nne, na mojawapo ilikuwa katika mwezi wa Rajab." Sisi hatukutaka kugombana na yeye. Tulikuwa tukimsikiya 'Aaisha (أم المؤمنين) akipiga mswaki (yaani; koromo za mswaki) kwenye chumba chake. 'Urwah akasema: "Ewe mamake Waumini, kwani hukumsikiya ayasemayo Abu 'Abdur-Rahmaan?" Akasema: "Asemaje?" Akasema: "Amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alifanya 'Umrah mara nne, na mojawapo ilikuwa ni katika mwezi wa Rajab." Akasema ('Aaisha): "Rehma za Allaah zimshukie Abu Abdur-Rahmaan, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kufanya 'Umrah yoyote isipokuwa yeye aliishuhudia [yaani; alikuwa pamoja nae], na wala hakuwahi kufanya 'Umrah katika mwezi wa Rajab." (Imeafikiwa).
Imepokewa na Imaam Muslim yakwamba ibn 'Umar aliyasikiya haya na wala hakusema "ndio" wala "laa". An-Nawawee amesema: "Uhakika kuhusu kunyamaza kwa ibn 'Umar 'Aisha alipokanusha aliposema inaashiriya yakwamba alitatizika, au alisahau, au hakuwa na hakika. Kwahiyo, ni bid'ah iliyozuliwa kuikusudia Rajab kwa 'Umrah na kuamini yakwamba kutekeleza 'Umrah katika mwezi wa Rajab ni jambo lenye fadhla maalum. Hakuna kitu kama hicho kilichopokewa, licha yakwamba haikupokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kufanya 'Umrah kabisa katika mwezi wa Rajab.

Amesema Sheikh 'Ali ibn Ibraahim al-'Attaar (k. 724 AH): "Miongoni mwa mambo ambayo niliyowahi kuyasikiya kuwahusu watu wa Makkah ni kwamba wao hufanya 'Umrah mara kwa mara katika mwezi wa Rajab. Hili ni jambo ambalo kwalo sijui limeegemezwa juu ya msingi gani, niyajuayo mimi ni kwamba imepokewa katika hadeeth yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "'Umrah katika mwezi wa Ramadhaan ni kama Hajj."
Amesema Sheikh Muhammad Ibn Ibraahim (رحمه الله) katika fataawa yake: "Amma kuhusu kupwekesha baadhi ya masiku ya Rajab kwa 'amali zozote nzuri, ziyaarah (kuizuru nyumba Tukufu ya Allaah - al-Ka'bah) au kitu chochote chengine, hakuna msingi wowote wa hayo, kwa sababu Imaam Abu Shaamah amesema katika kitabu chake *al-Bida' wa'l-Hawaadith*: "Kukhusisha vitendo vya ibada maalum katika nyakati ambazo hazikukusudiwa na sharee'ah ni makosa; hakuna wakati utakaofadhilishwa kuliko wakati mwengine isipokuwa katika hali ambayo sharee'ah imependekeza kwa kitendo maalum cha ibada katika wakati maalum, au kusema yakwamba kitendo chochote kizuri kinapofanywa katika wakati huu ni bora kuliko matendo mengi mazuri yaliyofanywa kwenye nyakati tafauti. Kwahiyo wanavyuoni wamepinga kitendo cha kuupwekesha mwezi wa Rajab kwa kufanya 'Umrah mara kwa mara.
Lakini ikiwa mtu atakwenda kufanya 'Umrah katika mwezi wa Rajab pasi na kuamini yakwamba jambo hili lina sampuli fulani ya fadhla na kwa sababu ilikuwa ni kwa bahati tu yakwamba ilikuwa kwake yeye ni jambo rahisi ende katika wakati huo, basi hapana makosa yoyote na hilo.

UZUSHI NA BID'AH KATIKA MWEZI WA RAJAB

Uzushi katika Dini ni mojawapo ya mambo yenye hatari yenye kwenda kinyume cha Kitaab cha Allaah na Sunnah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakufa mpaka baada ya dini hii kukamilika. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) (kulingana na tafsiri): **"... Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni ne'ema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu**

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

uwe dini yenu ..." [al-Maa'idah (5):3]. Imepokewa yakwamba 'Aaisha (رضي الله عنها) amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Yoyote mwenye kuzua katika jambo letu hili jambo ambalo lisilokuwemo, ataregeshewa mwenyewe.*" [imeafikiwa]. Kulingana na riwaya iliyopokewa na Muslim: "*Yoyote mwenye kufanya kitendo kisichokuwa katika jambo letu hili atakataliwa nalo.*"

Baadhi ya watu wamezua idadi kubwa ya mambo katika mwezi wa Rajab, yakiwemo yafuatayo:

SWALAAT *AR-RAGHAA'IB*

Swala hii imeenea baada ya Karne bora za mwanzo, hususan katika karne ya nne A.H. Baadhi ya watu warongo waliizua swala hii, ambayo hufanywa katika usiku wa mwanzo wa Rajab. Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله) amesema: "Swalaat *ar-Raghaa'ib* ni bid'ah kulingana na muafaka wa wanavyuoni katika dini kama vile Maalik, Ash-Shaafi'ee, Abu Haneefah, ath-Thawree', Al-'Auzaa'ee, al-Layth na wengineo. Hadeeth iliyopokewa kuhusiana na suala hilo ni urongo kulingana na muafaka wa wanavyuoni wenye 'ilmu ya hadeeth. Imepokewa yakwamba vituko vikubwa vilitokea katika mwezi wa Rajab, lakini hakuna riwaya ya kweli miongoni mwa vituko hivyo. Imepokewa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizaliwa katika usiku wa kwanza wa mwezi wa Rajab na kwamba alikabidhiwa Utume katika tarehe ya ishirini na saba, au ishirini na tano ya mwezi huu. Hakuna la kweli katika hayo. Imepokewa kwa isnaad ambayo sio swaheeh kutoka kwa al-Qaasim ibn Muhammad yakwamba safari ya usiku ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) (*al-Israa'*) ilitokea katika tarehe ishirini na saba ya mwezi wa Rajab. Haya yalikanushwa na Ibraahim al-Harbi na wengineo. Mojawapo ya mambo ya uzushi yaliyotokea katika mwezi huu ni usomaji wa kisa cha Mi'raaj, na sherehe ya kuikumbuka siku hiyo katika tarehe ya ishirini na saba ya mwezi huo, au kuupwekesha usiku huo kwa ajili ya kutekeleza vitendo vya ziyada vya ibada kama vile Qiyaam ul-Layl (kisimamo cha usiku) au kufunga saumu mchana wake, au kufurahi na kusherehekea. Baadhi ya sherehe ziandamana na mambo ya haraam kama vile kuchanganyikana wake kwa waume pasi na kuzuizi, kusikiliza miziki na nyimbo, yote ambayo yasiyoruhusiwa katika 'Eid mbili zilizofaradhishwa katika Uislamu, licha ya sherehe za uzushi. Ukiongezea juu ya hayo, ukweli yakwamba hapana dalili yoyote ya tukio hilo la Israa' na Mi'raaj kuwa yalitokea katika siku hiyo. Hata kama imethubutu, hapana dharura ya kufanya sherehe katika siku hiyo, kwa sababu hakuna mfano wake uliopokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au kutoka kwa Maswahaba zake (vizazi vya mwanzo) vya Umma huu. Lau kama lingelikuwa ni jambo zuri, kwa hakika wao wangelitutangulia sisi kwa hilo, twamuomba Allaah Atusaidie.

SWALAAT UMM-DAAWUD

[Katika nusu nzima ya Rajab]

* Du'aa zote zenye kusomwa hususan katika mwezi wa Rajab ni za kuzuliwa na Urongo.
* Kuzuru makaburi hususan katika mwezi wa Rajab ni bid'ah, kwa sababu makaburi yanafanyiwa ziyara katika wakati wowote bwa mwaka.

Twamuomba Allaah atuja'aliye tuwe ni miongoni mwa wale wenye kuyatukuza mambo ambayo Aliyoyafanya Yeye kuwa ni Matukufu na kushikamana na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa siri na kwa dhahiri, kwani Yeye ndiye wa Pekee wa kuombwa na Yeye ndiye Mwenye uwezo wa hayo. Na mwisho wa kufunga kwetu ni: Kutakasika ni kwake Yeye, Mola wa 'Aalameen (Binadamu na Majini na viumbe vyote).

FATAAWA

Hukmu Kuhusiana Na Kuharibika Kwa Mimba

Suali: Baadhi ya wanawake hupata msiba wa kuharibikiwa na mimba zao. Mara nyengine kiumbe kilichoanza kuumbika (kijusi) ndani ya tumbo lake hupatikana wakiwa wamekamilika na mara nyengine huwa hawajakamilika. Ningelipendelea utubainishie kuhusu hukmu ya swala katika hali zote mbili.

Jawabu: Ikiwa mwanamke akiharibikiwa na mimba na kijusi kikaonekana kuwa na umbo lilokamilika, kama vile kichwa, mikono, miguu na halkadhaalika, basi damu yake itakuwa ni damu ya mazazi. Atafuata hukmu ya damu ya mazazi. Hatoswali, hatofunga na wala mumewe hatoruhusiwa kuingiliana nae mpaka damu yake ikome kutoka au mpaka akamilishe siku arubaini. Ikiwa damu itakoma kabla ya siku ya arubaini, atawajibika kutekeleza josho la Ghusl, aswali, afunge mwezi wa Ramadhaan na mumewe ataruhusiwa kuingiliana nae.

Hakuna uchache wa muda wa wakati katika damu ya mazazi. Damu inaweza kukoma kutoka baada ya siku kumi, kuzidi au kupungua, kisha ni lazima atekeleze josho la Ghusl na atawajibika na sheriya zote za mtu alotwahirika. Iwapo ataona damu yoyote baada ya siku ya arubaini, itazingatiwa kuwa ni damu ya ugonjwa. Atafunga na kuswali na damu hiyo na itaruhusiwa kwa mumewe kuingiliana nae. Ni lazima atawadhe kila ifikapo wakati wa swala, kama Mustahaadhah, kama alivyosema Mtume(صلى الله عليه وسلم) kumwambia Faatimah bint Abu Hubaish (رضي الله عنهما): "*Tawadha katika wakati wa kila swala.*"

Ikiwa damu inayomtoka baada ya siku arubaini itapatana na wakati wa ada yake ya mwezi, basi itachukuwa hukmu ya heidh. Ni haramu kwake kuswali au kufunga mpaka atwahirike. Na ni haramu kwa mumewe kuingiliana nae.

Juu ya yote hayo, ikiwa atakachokizaa mwanamke hakilingani na umbile la mwanadamu, kama kwa mfano ikiwa ni pande nono la nyama au pande la damu, basi atafuata hukmu ya Istihaadhah na wala si hukumu ya damu ya mazazi. Ataswali, afunge mwezi wa Ramadhaan, na ataruhusiwa kuingiliana na mumewe. Atatawadha kila ufikapo wakati wa swala huku akijihifadhi na damu inayomtoka kwa surwale maalum au kitun chenye kufanana nayo, kama Mustahaadhah, mpaka damu isimame.

Pia anaweza kuunganisha swala ya Dhuhr na 'Asr pamoja na swala ya Maghrib na 'Ishaa' pamoja. Vilevile, anaweza kutekeleza josho la Ghusl kwa swala za kuunganisha na josho la Ghusl nyengine kwa swala ya Fajr kutokana na hadeeth iliyothubutu ya Hamnah Bint Jahsh (رضي الله عنهما). Hii ni kwa sababu atazingatiwa kuwa ni kama Mustahaadhah kulingana na Wanavyuoni.

Sheikh Ibn Baaz (رحمه الله)